



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BENKI KUU YA TANZANIA



13 Mei, 2024

TAARIFA KWA UMMA

**KATAZO LA KUJIHUSISHA NA BIASHARA YA KUKOPESHA KIDIGITALI BILA  
LESENI KUTOKA BENKI KUU YA TANZANIA**

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuufahamisha Umma kwamba chini ya kifungu cha 17 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, 2018, Benki Kuu ya Tanzania ina mamlaka pekee ya kutoa leseni kwa taasisi, makampuni, au watu binafsi wanaojihusisha na kutoa mikopo. Pia, kwa mujibu wa kifungu cha 16 (1) cha sheria hiyo, ni kinyume cha sheria kujihusisha na biashara ya kukopesha bila kuwa na leseni. Katazo hili linajumuisha utoaji wa mikopo kwa njia mbalimbali ikiwemo utoaji wa mikopo kwa njia ya Kidigitali bila kuwa na leseni.

Aidha, Benki Kuu inaukumbusha Umma kusoma kwa makini na kuelewa makubaliano wanayoingia na wakopeshaji, ikiwa ni pamoja na kuelewa masharti ya mikopo, na kuhakikisha kwamba mkopeshaji ana leseni halali ya kufanya biashara ya kukopesha. Mkopaji anapaswa kupewa nakala ya mkataba uliosainiwa kwa njia sahihi, na nakala hiyo inapaswa kutolewa kila mkopeshaji anapotoa mkopo mpya.

Benki Kuu inaendelea kuusisitiza Umma kujiepusha kufanya biashara na taasisi, makampuni, au watu binafsi wanaotoa huduma za kukopesha bila kuwa na leseni halali iliyotolewa na Benki Kuu. Aidha, Umma unaombwa kutoa taarifa Benki Kuu na vyombo vya usalama juu ya taasisi, makampuni au watu binafsi wanaofanya biashara bila kuwa na leseni au kutozingatia taratibu zilizowekwa kwa ajili ya kuchukuwa hatua za kisheria. Benki Kuu imetoa orodha ya taasisi, makampuni, na watu binafsi walio na leseni za biashara za kukopesha kwenye tovuti yake: [www.bot.go.tz](http://www.bot.go.tz).

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:- Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Idara ya Usimamizi wa Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, S. L. P 2939, 11884 Dar es Salaam, Simu Na. +255 22 223 5585; Barua Pepe: [info@bot.go.tz](mailto:info@bot.go.tz) or [botcommunications@bot.go.tz](mailto:botcommunications@bot.go.tz).

Emmanuel M. Tutuba

GAVANA

**BENKI KUU YA TANZANIA**